**Learning by Ear 2011 – Usalama Barabarani**

**Episode 01 – Mikanda ya Usalama**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Martin Vogl**

**CHARACTERS:**

Onyesho la 1:

- MSOMAJI HABARI (MWANAMKE AU MWANAMUME)
- SAMUEL (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 30-40)
- PAMELA (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 30-40)
- ALICE (MSICHANA, UMRI WA MIAKA13, Binti yao Pamela na Samuel)

Onyesho la 2:

- SAMUEL (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 30-40)
- ROBERT (MWANAMUME, UMRI WA 30-40, Dreva msaidizi wa Samuel)
- NELSON (MVULANA, UMRI WA MIAKA 14, Mwanao Pamela na Samuel)

Onyesho la 3:

- SAMUEL (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 30-40)
- ASKARIPOLISI (MWANAMUME)

Intro/Studio/Outro:

- MTANGAZAJI BEATRICE (MWANAMKE)

- GEORGE – MTAALAMU WA USALAMA BARABARANI (MWANAMUME)

Tah: Mtangazaji anaweza kuwa mwanamume na mtaalamu wa usalama barabarani anaweza kuwa mwanamke.

**Intro:**

**1. Beatrice:** Karibuni kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha yako na kwenye michezo yetu ya redio kuhusu usalama barabarani. Mtangazaji wako ni mimi Beatrice. Kwenye vipindi kumi vitakavyofuata tutaandama na familia ya Wanjiru. Tutaangazia maisha yao ambapo walishuhudia maafa yanayotokana na ukosefu wa usalama barabarani barani Afrika. Baadaye tutazungumza na mtaalamu wa usalama barabarani ili tufahamu vile ambavyo tunaweza kuhakikisha usalama barabarani ili kuokoa maisha ya watu. Katika kipindi cha kwanza cha mchezo wetu wa redio tunawapa familia ya wanjiru nyumbani: Samuel ambaye ni dereva wa basi, mke wake Pamela, na watoto wao watatu Nelson, Alice na Matthew.

**Scene One: in the family home**

**2. TV NEWSREADER:** Serikali leo imetangaza taratibu za kuimarisha usalama wa barabara zetu. Hatua hiyo imechukuliwa kutokana ajali nyingi zilizosababisha maafa makubwa katika kipindi cha sikukuu ya Krismasi. Mojawapo wa hatua za kwanza ni kupitisha sheria kwa magari yote - ya umma nay a kibinafsi - kuwa na mikanda ya usalama kwa abiria wote. Wataokosa kujifunga mikanda hiyo watachukuliwa hatua za kisheria...

**3. SFX:** **turning TV off**

**4. SAMUEL:** Hilo haliingii akilini! Hebu nambie unadhani itachukua muda na fedha kiasi gani kuweka matatu na mabasi yote mikanda ya usalama?! Ina maana kwamba nitakaa kwa siku kadha bila kipato... pengine hata mwenye gari hawezi kuweka mikanda ya uslama maana naye pia atagharamika... Pia basi litakuwa na viti vichache iwapo kila abiria atalazimika kujifunga mkanda. Gharama zaidi hiyo! Hili jambo linaingia akilini kweli Pamela?

**5. PAMELA:** Samuel, mimi sijui. Mara nyingine naogopa jinsi nyinyi madereva wa matatu mnavyoendesha magari mfano wa wendawazimu. Wanaendesha magari kwa kasi huku wakishindana mabarabarani. Wengi wao hawawajali watembea kwa miguu wanaotembea kando kando ya barabara. Mara ngapi nusura nigonge kioo cha mbele cha gari pale dereva anaposimamisha gari ghafla! Wala abiria hawathubutu kuwaambia madereva kuendesha magari taratibu - wanaogopa...

**6. ALICE:** Kweli mama! Natamani kungekuwa na mtu wa kumwambia dereva kupunguza kasi. Niliwahi kupanda basi lenye mikanda ya usalama – lakini hakuna hata mmoja aliyejifunga mkanda.

**7. SAMUEL:** Ndiyo hivyo, hakuna yeyote anayejifunga mikanda, basi kuna haja gani kuwa nayo, Alice?

**8. ALICE:** Bila shaka, wanaohusika wanaelewa kuwa ni bora kujifunga mikanda ya usalama. Vinginevyo wasingeweka sheria hiyo ya mikanda…

**9. SAMUEL:** **(angry)** Njia nyingine tu ya kujipatia fedha kutoka kwetu. Nakwambia mikanda ya usalama haina kazi! Kama nikupata ajali, unaipata vivyo hivyo. Wala hiyo mikanda haikusaidii kitu. Tuyaache hayo. Nataka kwenda kazini. (anamwambia Nelson): Nelson, fanya bidii, inatubidi kuaharakisha! (wanaondoka): Tutaonana baadaye.

**10. SFX:** **sound of door shutting**

**<u>Scene two: on the roads</u>**

**11. SFX:** **street sounds, cars, horns blaring**

**12. SFX:** **a mini-bus revs its motor, engine keeps on running the whole scene**

**13. SAMUEL:** Robert jitahidi, mchukue abiria yule – twatakikana kuanza safari. Tazama lile basi limetupita na linakwenda kutwaa lile kunde pale... harakisha!

**14. ROBERT:** HAYA, HAYA, Ingia ingia, songeni nyuma, kuna nafasi ya mtu mmoja katika kiti kile, songeni. Nauli mkononi tafadhali...

**15. SFX:** **Noise of coins in Roberts hand**

**16. SFX:** **sound of mini bus revving and moving off**

**17. NELSON:** Baba, leo unaendesha basi kwa kas i- mbona unaonekana kama mtu ambaye amenuna?

**18. SAMUEL:** Nelson, sijanuna. Ninataka nifanye kazi leo ili nipate fedha nyingi iwezekanavyo – inanibidi nilipe karo yako ya shule yote kufikia juma lijalo. Kwa hivyo ni lazima nibebe abiria wengi.

**19. NELSON:** Sawa, baba! Naona unaendesha kwa kasi na hivi sana mvua inanyesha na tena kuna mashimo mengi barabarani... Baba, Chunga hilo shimo kubwa!

**20. SFX:** **sound of cars swerving and a loud bang as the mini bus crashes**

**Scene three: crash site**

**21. SFX ATMO:** **Sound of people wailing and crying, police sirens**

**22. SAMUEL:** Mungu wangu, kumetokea nini? Basi langu limefanyika nini? Nelson yuko wapi? Mwanangu?!? Mwanangu!!! Nelson!!! **(getting increasingly desperate)**

**23. POLICEMAN:** Tulia. Tafadhali!

**24. SAMUEL:** Mwanangu! Ninamtaka mwanangu!!!

**25. POLICEMAN:** Tulia! Tutampata mwanao. Lakini kwanza tulia. Ulikuwa umepoteza fahamu. Umepata ajali na nusura urushwe kutoka kwenye basi lako ulipoligonga lile gari jingine. Usukani ndio pengine uliokuzuia. Abiria watano walirushwa kutoka kwenye basi. Wawili wamefariki na watatu wanapelekwa hospitalini. Shukuru Mngu kwamba umenusurika.

**26. SAMUEL:** Mungu wangu. Mwanangu yu wapi? Ni lazima nifike hospitalini.

**27. POLICEMAN:** Bora uende hospitalini ukachunguzwe kichwa chako hicho – mwili wako umejaa damu. Ulikuwa umezimia. Lakini kwa kuwa wewe ndiye dereva wa basi hilo, baadaye hii leo tutakuhoji na kuchunguza nyaraka zako zote.

**28. SAMUEL:** Maskini, watu wamefariki? **(starts crying)** Lakini, mvua ilikuwa ikinyesha… Sikuliona hilo shimo… **(screaming desperately)** La, la, la!!! Nimefanya nini mimi???

**29. POLICEMAN:** **(authoritative)** Tulia, tafadhali! Hii ilikuwa ajali mbaya sana. Una bahati kwamba hukuwaua watu waliokuwa kwenye gari hilo jingine. Wote walikuwa wamejifunga mikanda ya usalama. Na walikutoa kwenye basi lako baada ya kusababisha hiyo ajali na kupoteza fahamu. Sasa twende hospitalini. Tutaandamana na wewe hadi huko. Baada yako kupata matibabu tutashughulikia nyaraka zako na pia utaandikisha taarifa.

**END OF SCENE THREE**

**SHORT MUSIC**

**30. BEATRICE:** Naam, kama mlivyosikia katika kipindi hicho cha kwanza cha mchezo wetu wa redio kuhusu usalama barabarani, ni siku ya huzuni kwa familia ya Wanjiru. Lakini je hatua gani zingechukuliwa kuepukana na ajali kama hiyo? Hapa studioni ninaye mtaalamu wa usalama barabarani mgeni,Bwana George, tutajadiliana jinsi tunavyoweza kubadilisha mfumo wa maisha yetu nakuweza kuwa na usalama katika mfumo wa usafiri barabarani. Karibu George!

**31. GEORGE:** Asante sana, Beatrice. Ninaposikiza kipindi hicho cha mchezo wa redio kinanitanabahisha kuhusu jinsi ninavyokwenda kazini kila siku. Jambo la kwanza ninalofanya ninapoingia kwenye gari langu ni kufunga mkanda wa usalama. Ni jambo ambalo limekuwa ada wala siwezi kusahau. Kusema kweli nisipofanya hivyo sina raha hata kidogo!

**32. BEATRICE:** Je umekuwa ukijifunga mikanda ya usalama?

**33. GEORGE:** Ndio na hapana. Kila niliposafiri pamoja na wazazi wangu walinishurutisha kujifunga mkanda wa usalama – tangu nikiwa mtoto mdogo. Lakini mambo ni magumu kwenye usafiri wa umma. Kama tulivyosikia, matatu na mabasi mengi hayana mikanda ya usalama, na kama yanayo, mikanda yenyewe haifai. Na mara nyingine unapopanda teksi madereva wanakushauri kutoitumia mikanda hiyo.

**34. BEATRICE:** Je ni wazo zuri kuwa na sheria ya kuwashurutisha watu kujifunga mikanda ya usalama?

**35. GEORGE:** Bila shaka. Katika Ulaya na Marekani kwa muda wa miaka mingi kumekuwa na hiyo sheria na usipojifunga mkanda unapokaa kiti cha mbele au cha nyuma kwenye gari unaweza kutozwa faini au hata kutiwa nguvuni. Nadhani ndiyo njia ya pekee ya madereva na wenye magari kuhakikisha kuwa magari yao yana mikanda ya usalama inayofaa. Hasa wanapojuwa kwamba kukosa mikanda kutawasababisha kutozwa faini au kukamatwa. Kabla ya mikanda ya usalama kutangazwa kuwa lazima nchini Ujerumani mwaka 1984, idadi chini ya nusu ya abiria ndio waliokuwa wakijifunga mikanda hiyo wakiwa mijini. Miaka michache baada ya sheria hiyo kupitishwa na askari polisi wakaanza kuwatoza wasafiri faini, takribani asili miaka 90 ya watu walianza kujifunga mikanda yao ya usalama.

**36. BEATRICE:** Hata hivyo George, je kuna ithibati yoyote kwamba matumizi ya mikanda ya usalama yanahakikisha usalama wa wasafiri?

**37. GEORGE:** Ndio, mara kwa mara hukaguliwa na pia mifano hutolewa kuonyesha jinsi matumizi ya mikanda hiyo yanavyosaidia kupunguza maafa wakati wa ajali Pia mambo mengine kama vile kuendesha gari kwa kasi, mtu kuwa makini anapoendesha gari na kadhalika, lakini kujifunga mkanda wa usalama ni mojawapo ya mambo muhimu zaidi.

**38. BEATRICE:** Lakini mikanda ya usalama inasaidiaje kuhakikisha usalama wa usafiri?

**39. GEORGE:** Unapojifunga mkanda wa usalama, unajipunguzia hatari ya kufa au kujeruhiwa vibaya endapo ajali itatokea. Ebu fikiria iwapo hujafunga mkanda wa usalama, unaweza kurushwa nje ya dirisha au – iwapo umekaa nyuma bila mkanda wa usalama - huenda ukarushwa upande wa kiti cha mbele kwenye gari. Mkanda wa usalama unakukinga na kukuzuia usidhurike zaidi. Kwa hivyo inampasa kila mtu kujifunga. Jifunge mkanda kila mara unapopanda gari, taxi au matatu!

**40. BEATRICE:** Asante sana George kwa kutembelea studio zetu.

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**OUTRO**

**41. BEATRICE:** Katika kipindi kitakachofuata tutajua yaliyomtendekea Nelson. Pia tutasikia jinsi familia ya Wanjiru inavyonusurika kupata ajali nyingine kutokana na kasi za madereva katika mchezo mwengine wa redio ulioandikwa na Victoria Averill. Ukitaka kukisikiliza kipinid hiki tena, tafadhali tembelea wavuti yetu www.dw.de/lbe. Tunakushukuru kwa kuungana nasi na kuhakikisha kuwepo usalama barabarani!